

# KILA DAKIKA TUMFIKIRIE MRENO — ASEMA CHAMATU

Mwandishi wetu, Tanga, Alhamisi.

**M**WANA-MSUMBIJI ye yote ambaye anakaa kwa dakika hata moja tu bila kuwaza jinsi ya kupata uhuru wa nchi yake ya Msumbiji inayotawaliwa na Mreno basi anampa nafasi zaidi Waziri Mkuu wa Ureno, Salazar kudumisha milki yake katika nchi hiyo.

Hayo yalisemwa katika mkutano wa hadhara na Mwandishi wa Jimbo la Tanga wa chama cha watoro wa Msumbiji (FRELIMO), Bw. F.M. Chamatu, kwenye uwanja wa Masiwani juzi.

Kiongozi huyo alisema kwa-mba Ureno imekuwa ikitawala Msumbiji bila idhini ya wananchi kwa muda wa miaka 468 sasa. na inawapasa Wareno kutambua kuwa wakati wao wa kuondoa ufalme wao umewadia.


"Tunaishukuru Serikali ya Tanganyika." alisema Bwana Chamatu, "kwa kutuletea Dr. Mondlane, pia mwana-Msumbiji, kutoka Amerika kuja kuongoza chama cha watoro wa nchi yetu hapa Tanganyika, maana sisi tunaamini kwamba yeye ndiye kiongozi wa kufaa kupambana na kuondolewa kwa ukoloni wa Mreno katika nchi yetu", alitanka.

## Wake 50

Kiongozi huyo aliwaonya wananchi wa Msumbiji sasa kutupilia mbali mipango ya kuoqa wanawake zaidi ya 30, na akaonya kwamba fahari hiyo wakati wake ulipita, na fahari ya sasa ambayo wananchi wote imewakabili ni ile ya kupambana na ukatili wa utawala wa Kireno katika nchi ya Msumbiji.

"Tusimwache Mreno azidi kujitajirisha katika nchi yetu, maana maadamu anatambua kwamba sasa wakati wake wa kuondoka umefika, anafanya kila juhudi kuchukua utajiri wa nchi hiyo kupeleka kwake na kutuacha masikini wakati ataondoka", alisema Bwana Chamatu.

"Ama mimi ningekuwa na



madaraka kama ya kiserikali," aliongeza kupasua kiongozi huyo, "ningemlazimisha kila mwananchi mtoro kutoka Msumbiji anayeishi katika Tanganyika kukata kadi ya TANU".

Wakati mkubwa wa hotuba yake kiongozi huyo alisisitiza juu ya kutaka kuweko umoja thabiti wa wananchi wa Msumbiji.

Nchi zote za ulimwenguni, aliongeza, isipokuwa zile ambazo zimo katika Umoja wa NATO, zinapendelea na kujihudisha kuisaidia Msumbiji kujipatia uhuru wake.

"Na umoja wa nchi za

## Hawatavumilia

Afrika," aliendelea Bw. Chamatu, "hautavumilia tena kumwachilia Mreno azidi kuitawala Msumbiji."

Alisema Umoja huo utafanya kila juhudi kuuondoa utawala wa Kireno, "hata kama sisi wenyewe wa Msumbiji tatalala juu ya juhudi hizi."

Hivi sasa kiongozi wa kundi la vijana wa Frelimo, Bwana K. Dewas, pamoja na Bwana Chamatu, wamo katika ziara ya kutembelea sehemu mbali

mbali ambako watafanya mkutano wa hadhara kuwahutubia wananchi wa Msumbiji wanaoishi katika Jimbo hili la Tanga.